

**HOTUBA YA MHESHIMIWA QUEEN CUTHBERT SENDIGA,
MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA MAADHIMISHO
YA SHEREHE ZA MUUNGANO TAREHE 26 APRILI, 2023.**

- **Katibu Tawala Mkoa,**
- **Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (MNEC),**
- **Kaimu Katibu wa CCM Mkoa,**
- **Kamati ya Usalama Mkoa,**
- **Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**
- **Wahe. Wabunge,**
- **Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo Sekretarieti ya Mkoa,**
- **Wakuu wa Taasisi za Umma na Binafsi,**
- **Makatibu Tawala wa Wilaya,**
- **Viongozi wa Vyama vya Siasa,**
- **Mstahiki Meya,**
- **Wenyeviti wa Halmashauri,**
- **Wakurugenzi wa Halmashauri,**
- **Waheshimiwa Madiwani,**
- **Wakuu wa Idara za halmashauri,**
- **Watumishi wa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri,**
- **Baraza la Wazee Mkoa na Wilaya,**
- **Baraza la Machifu,**
- **Viongozi wa Kamati ya Amani ya Mkoa,**

Marais wengine wote waliopita kwa kuendeleza muungano wetu pamoja na Rais wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendeleza yale mazuri ya muungano na kutatua kero mbalimbali za muungano

Ndugu Wananchi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa tarehe 26 Aprili, 1964 ikiwa ni Muungano wa Mataifa mawili huru ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ambayo yaliingia Mkataba wa Muungano mnamo mwaka 1964 na kuanzishwa Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkataba wa Muungano ulitiwa Saini na aliyekuwa Rais wa Tanganyika Hayati Mwalimu Julius Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar Hayati Sheikh Abeid Aman Karume tarehe 22 Aprili, 1964 huko Zanzibar. Mkataba huo ulithibitishwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi tarehe 26 Aprili, 1964 na tarehe 27 Aprili, 1964 viongozi wa nchi zote mbili walikutana katika ukumbi wa Karimjee Jijini Dar es Salaam na kubadilishana Hati za Muungano.

Ndugu Wananchi, Kama mnavyofahamu kuwa leo tarehe 26 Aprili, 2023 wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Watanzania tunashuhudia Muungano wetu ukitimiza miaka 59 ambayo umekuwa ni wenyе mafanikio makubwa ambayo yamenufaisha wananchi katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Muungano umewapa fursa wananchi wa pande zote

Makamu wa Rais imeendelea kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hivyo kuendelea kuimarisha mashikamano na udugu wa pande zote za Muungano.

Ndugu Wananchi, Mkoa wetu ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unashuhudia mafanikio makubwa ya muungano wetu ambayo ni uwepo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotambua uwepo wa Muungano. Pili ni kuimari kwa ulinzi na usalama wa nchi yetu ambapo wananchi wa pande zote mbili za Muungano wameendelea kuishi kwa Amani na Utulivu. Faida nyingine ni pamoja na wananchi kutumia fursa za muungano za kijamii ambapo wananchi wamejipatia fursa ya makazi, biashara, haki za uraia, elimu na ajira kwa ajili ya kujitafutia maendeleo kupitia taasisi za muungano kama vile Bodi za Mikopo ya Elimu ya Juu ambapo wanafunzi wenyewe sifa wa kutoka Mkoa wa Rukwa pia wamekuwa wakinufaika kwa kupatiwa mikopo ya kugharamia masomo yao ya Elimu ya Juu.

Ndugu Wananchi, Kwa kufurahia matunda ya uraia wa nchi moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wananchi wamekuwa na uwezo wa kwenda au kuishi sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kutumia hati za kusafiria. Kumekuwa na mwingiliano wa Tamaduni kama aina

- (iii) Kuendelea kuboresha Elimu yetu ambapo jumla ya Shilingi Bilioni 33 zimeletwa katika kipindi cha miaka miwili kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Elimu katika kipindi hiki cha miaka miwili ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- (iv) Huduma za Afya katika kipindi cha miaka miwili ya Rais Samia zimeendelea kuboreshwa ambapo tumepokea Shilingi Bilioni 8.4 kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati, Vituo vya Afya na umaliziaji wa Hospitali za Wilaya. Aidha, vifaa mbalimbali vya Hospitali na Vituo vya Afya vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.4 vimenunuliwa.
- (v) Upande wa kilimo tunapoahimisha miaka 59 ya muungano tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mbolea ya Ruzuku kwa kutoa Shilingi Bilioni 150 kwa ajili ya Ruzuku ambapo katika msimu huu wa kilimo wananchi wanatarajia kuvuna Tani Milioni 1.6 ya mazao ya chakula na Biashara ambapo mahindi pekee tunatarajia kuvuna tani laki saba. Aidha, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanalima kilimo cha uhakika cha umwagiliaji tumepokea jumla ya Shilingi Bilioni 21 kwa ajili ya ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya llemba. Aidha, Skimu ya Lwafi/Katongolo usanifu wake unaendelea kwa ajili